ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Jimbo la Mahonda
2.	Mhe.	Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
3.	Mhe.	Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
4.	Mhe.	Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
5.	Mhe.	Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
6.	Mhe.	Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
7.	Mhe.	Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
8.	Mhe.	Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
9	Mhe.	Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
10.	Mhe.	Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
11.	Mhe.	Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
12.	Mhe.	Chum Kombo Khamis	-	Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	Jimbo la Tumbatu
14	Mhe.	Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
15.	Mhe.	Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
16	Mhe.	Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
17.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	Jimbo la Makunduchi
18.	Mhe.	Harusi Said Suleiman	-	Jimbo la Wete
19	Mhe.	Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
20.	Mhe.	Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
21.	Mhe.	Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
22.	Mhe.	Issa Haji Ussi (Gavu)	-	Jimbo la Chwaka
23.	Mhe.	Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
24	Mhe.	Juma Makungu Juma	-	Jimbo la Kijini
25.	Mhe.	Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
26	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	Jimbo la Donge
27.	Mhe.	Khamis Juma Mwalim	-	Jimbo la Pangawe
28.	Mhe.	Lulu Msham Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
29.	Mhe.	Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
30.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	Jimbo la Kiembesamaki
31.	Mhe.	Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
32.	Mhe.	Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
33	Mhe.	Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando

34	Mhe.	Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
35.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Nafasi za Wanawake
36.	Mhe.	Mihayo Juma N'hunga	-	Jimbo la Mwera
37.	Mhe.	Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
38.	Mhe.	Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Jimbo la Mkoani
39.	Mhe.	Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
40.	Mhe.	Mohamed Ahmada Salum	-	Jimbo la Malindi
41.	Mhe.	Mohammed Said Mohammed	-	Jimbo la Mpendae
42.	Mhe.	Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini
43.	Mhe.	Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
44.	Mhe.	Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
45.	Mhe.	Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
46.	Mhe.	Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
47.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Jimbo la Chukwani
48.	Mhe.	Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
49.	Mhe.	Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
50.	Mhe.	Dkt Mwinyihaji Makame Mwadin i	-	Jimbo la Dimani
51.	Mhe.	Nadir Abdul-latif Yussuf	-	Jimbo la Chaani
52	Mhe.	Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
53.	Mhe.	Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
54.	Mhe.	Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
55.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	Jimbo la Amani
56.	Mhe.	Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
57.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	Nafasi za Wanawake
58.	Mhe.	Saada Ramadhan Mwenda	-	Nafasi za Wanawake
59.	Mhe.	Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
60.	Mhe.	Salama Aboud Talib	-	Nafasi za Wanawake
61.	Mhe.	Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
62.	Mhe.	Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
63.	Mhe.	Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
64.	Mhe.	Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
65.	Mhe.	Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
66.	Mhe.	Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
67.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Jimbo la Mgogoni
68.	Mhe.	Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
69.	Mhe.	Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
70.	Mhe.	Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake

71.	Mhe.	Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
72.	Mhe.	Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
73.	Mhe.	Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
74.	Mhe.	Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
75.	Mhe.	Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
76.	Mhe.	Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
77.	Mhe.	Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

	Dkt. Yahya Khamis Hamad	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KWANZA

Kikao cha Pili - Tarehe 1 Aprili, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika: (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kifungu cha 84 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaeleza kwamba katika mamlaka ya shughuli zake Rais wa Zanzibar atahusika kulihutubia Baraza la Wawakilishi wakati wowote atakaona unafaa kufanya hivyo. Chini ya Kanuni ya 21 (9) ya kanuni za Baraza toleo la 2012;" Endapo Rais atatoa taarifa kwa Spika kwamba anakusudia kutoa hotuba ya ufunguzi wa Baraza Spika, atalitangazia ni wakati gani Rais atalihutubia Baraza".

Kwa hivyo, basi naomba kutoa taarifa kwamba nimepokea rasmi kuhusu ujio wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Moh'd Shein kulihutubia Baraza la Wawakilishi. Taarifa yenyewe inasomeka kama ifuatavyo:-

"Kwa heshima nakuarifu kwamba kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya kifungu cha 84 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Moh'd Shein ameamua kulihutubia Baraza la Wawakilishi siku ya Jumanne tarehe 5 Aprili, 2016 saa 4 asubuhi. "

Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwasilisha taarifa hiyo kwenu. (*Makofi*)

UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa kazi iliyopangwa katika *order paper* inayofuata ni shughuli za uchaguzi wa Naibu Spika. Kwa hiyo nitaomba sasa Makatibu waweke utaratibu, tuingie kwenye hii shughuli ambayo nayo ni muhimu.

Katibu: Mhe. Spika, sasa tunaingia katika hatua ya uchaguzi wa Naibu Spika, na baadae uchaguzi wa wenyeviti. Kanuni zetu hazisemi kwamba lazima tuchague tafauti yaani uchaguzi uende mmoja baada ya mmoja. Kwa maana hiyo tungependekeza pia Waheshimiwa kama mtakubali basi tufanye chaguzi hizo kwa pamoja. Kwenye uchaguzi wa Naibu Spika tumepata jina la mgombea mmoja tu kutoka kwenye Chama cha Mapinduzi ni Mhe. Mgeni Hassan Juma, tayari amejaza fomu za uteuzi za Baraza kwa ajili ya uchaguzi huu na ameungwa mkono tayari na Wajumbe, ili asimame kuwa ni mgombea. (*Makofi*)

Kwa hiyo, baada ya maelezo haya tutamuomba Mhe. Mgeni Hassan Juma aje kutoa maelezo mafupi kwa Wajumbe kabla ya zoezi la kumpigia kura. Kwa sababu mgombea ni mmoja tu kura zitakuwa za ndio au hapana.

Kwenye nafasi za wenyeviti, tumepokea majina na nafasi kama tunavyojua za wenyeviti ni mbili na tumepokea majina mawili tu kutoka Chama cha Mapinduzi kuwa ni wagombea wa nafasi hizo. Waheshimiwa hao ni Mhe. Riziki Pembe Juma na Mhe. Shehe Hamad Mattar. Kwenye *ballot* yao yaani yataonekana majina mawili hayo; la kwanza na la pili na mbele huku kutakuwa na alama za ndio na hapana. Kwa hiyo, kila sehemu ya kulia ya mstari utaweka kwenye alama mmoja ama ni ndio au hapana kwa wagombea hawa wawili.

Baada ya maelezo haya Mhe. Spika, na kwa ridhaa yako naomba kwanza umwite Mhe. Mgeni Hassan Juma aje kutoa maelezo mafupi yasiozidi dakika tano na ambapo Wajumbe wataweza kumuuliza masuala na baadae hivyo hivyo uwaite Waheshimiwa wengine hawa wawili kwa ajili ya nafasi ya Uwenyekiti halafu kama mtatukubalia na

rai yetu Mhe. Spika, mturuhusu tugawe *ballot* zote kwa pamoja kura zipigwe kwa pamoja na tutazikusanya tofauti. Tutakusanya kwanza ya Mhe. Naibu Spika, na baadae tutakusanya zile za wenyeviti tuende kuzihesabu kwa pamoja na baadae tuje kutoa matokeo kwa pamoja. (*Makofi*)

Baada ya uchaguzi Mhe. Spika, kwa sababu Wajumbe hawa tayari wameshaapa kiapo cha uaminifu hawatatakiwa kuapa tena kiapo cha nafasi hizi. Kwa hiyo, baada ya zoezi hilo tutakuwa tumemaliza zoezi letu Mhe. Spika. (*Makofi*)

Sasa kwa heshima na taadhima Mhe. Spika, naomba umwite Mhe. Mgeni Hassan Juma kwa ajili ya kuendelea na hatua nilizozielekeza. Nashukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Karibu Mhe. Mgeni Hassan Juma, kama una lolote la kuwaeleza Wajumbe na kama kuna maswali ya kuyajibu matatu nitawaruhusu Wajumbe wakuulize. Tafadhali.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Wajumbe mlioko hapa wote *Assalam Alaykum*.

Kwanza awali ya yote nimshukuru "*Sub-hanahuu Wataala"* alietujaalia kufika hapa tukiwa wazima wa afya. Ndugu zangu Wajumbe, mimi sitakuwa na mengi ya kusema; kwanza kwa sababu naamini wengi mnanifahamu na wengi mmeniona nikifanya kazi katika nafasi ya uenyekiti. (*Makofi*)

Hivyo basi naomba mnipe ridhaa yenu ili kwa kipindi hiki cha 2016 - 2020 niweze kutumikia nafasi ya Unaibu Spika. Nimechagua nafasi hii kwa sababu najiamini, ninaweza lakini na kwa sababu nimeona umefika wakati na mimi niweze kuchangia katika kuliendeleza Baraza hili ili liweze kuleta manufaa katika Taifa letu.

Kwa hiyo, ndugu zangu kwa heshima kubwa nimesimama hapa naomba mnipe kura zenu zote na naahidi sitawaangusha. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mgeni Hassan Juma. Waheshimiwa Wajumbe kama kuna Mjumbe yeyote ambaye ana suali anataka kuuliza, naona kuna mkono kule nyuma Mhe. Hamza Hassan Juma, tafadhali.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza suala Mhe. Mgeni Hassan Juma mgombea wetu wa nafasi ya Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma alikuwa Mjumbe wangu wa kamati ya kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa kitaifa kwa muda wa miaka miwili na nusu na inaonesha ni mtu ambaye anajifunza kwa haraka sana. Kwa sababu ndani ya miaka miwili ameweza akachaguliwa baada ya miaka miwili na nusu ya kamati ameweza kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa kamati akawa Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Lakini vile vile Mhe. Spika, kabla ya kuja na suala kwa sababu najenga hoja Mhe. Mgeni Hassan Juma pia amechaguliwa katika kipindi kilichopita kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Baraza la Wawakilishi yaani UWAWAZA na jumuiya hii ameijenga sana kitaalamu na kila kitu sasa .....

Mhe. Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma samahani ningeomba tukaenda kwenye suala moja kwa moja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, Sasa kwa kuwa Jumuiya ya UWAWAZA ameweza kuiongoza katika umahiri mkubwa na sasa hivi anagombea nafasi ya Unaibu Spika. Je, hii nafasi ambayo aliijenga na akawajenga sana Waheshimiwa wanawake atamuachia nani katika kipindi hiki. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuniuliza suala ambalo mara nyingi liliulizwa na Wajumbe wengi hata mpaka wafanyakazi wa Barazani.

Mimi nataka kumwambia Mhe. Hamza Hassan Juma kwa bahati nzuri sana Wajumbe wanawake safari hii wamekuwa wengi ukilinganisha na idadi ya kipindi kilichopita na naamini kabisa wakati mimi nitachukuwa jukumu la Unaibu Spika, naamini kabisa kuna wengine wanaweza kujitokeza kwa uenyekiti wa UWAWAZA. Kwa sababu nimeshaona kwamba wapo ambao wanauwezo mkubwa wa kuendesha shuhuli mbali mbali zilizomo ndani ya Baraza letu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mhe. Hamza Hassan Juma pia nataka kukwambia kwamba kwa sababu nitakuwepo katika nafasi ambayo itanipa vile vile uwezo wa kusaidiana na wenzangu ambao watachukuwa nafasi hizo za UWAWAZA basi nawaambia hasa wanawake kwamba nitatoa ushirikiano wangu wa hali ya juu ili kuhakikisha kwamba UWAWAZA inaendelea. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mgeni Hassan Juma. Waheshimiwa Wajumbe kama kuna mwengine yeyote mwenye suali. Ahsante sana Mhe. Mgeni Hassan Juma. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe nadhani tumekubaliana kwamba baada ya kujieleza Mheshimiwa ambaye anagombea nafasi ya Unaibu Spika tuwape pia nafasi Waheshimiwa ambao wanagombea nafasi za Uenyekiti wa Baraza la Wawakilishi na wao kabisa wajieleza ili tutakapopiga kura tupige zote kwa wakati mmoja kabla ya kuakhirisha na kwenda kusubiri matokeo.

Sasa basi nachukuwa nafasi hii kwa heshima kabisa namwita Mhe. Riziki Pembe Juma, tafadhali Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Riziki Pembe Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Kiongozi wa shughuli za Serikali Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi, *Assalam alaykum*.

Kwanza kabisa na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai, uzima na afya njema na kuweza kukutana hapa leo hii tena kwa mara ya pili ndani ya ukumbi huu wa Baraza. Mimi nasema mara ya pili kwa sababu mimi mara yangu ya pili kuingia ndani ya huu ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, pamoja na Waheshimiwa wenzangu kama ambavyo nimeeleza awali naitwa Riziki Pembe Juma, ninagombea nafasi ya Uenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, wengine wataona kwamba ni sura ngeni ya Baraza ila si ngeni ndani ya jamii ya Zanzibar. Kwa hiyo, naomba kugombea nafasi hii nikiwa nina imani kwamba nitaiweza, nitaimudu na nitaweza kufanikisha yale malengo ya Baraza letu la Wawakilishi. Lakini zaidi ni kwamba tutaweza kujenga ule mustakbali wa kuwasaidia wananchi wetu wa Zanzibar ambao wao ndio waliotuleta humu ndani.

Kwa hiyo, kwa imani hiyo naomba sana Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi mnipe imani yenu na muamini kwamba hiyo nafasi mtakuwa hamjaitupa bali itakuwa mumeweka nafasi kwa mtu sahihi ambaye atakaekuwa anaweza kufanya hilo jukumu. Kwa hiyo, nawahakikishia kwamba *inshaallah* nitafanya kazi zangu kwa uadilifu. Lakini pia nitakuwa tayari kupokea maelekezo na mafundisho kwa sababu kama nilivyosema awali ni mara yangu ya kwanza ndani ya Baraza la Wawakilishi ila si mara ya kwanza kufanyakazi kama hizi.

Kwa hiyo, nina imani kwamba mtanipa mashirikiano mazuri pamoja na Mhe. Spika, akiwepo hapa kwa hiyo tutasaidiana na Baraza letu litaweza kwenda vizuri na yale maendeleo, matarajio na imani za wananchi wa Zanzibar kwamba Baraza la Wawakilishi liko vizuri na tunaweza kufanya kazi hiyo na tukawakilisha vizuri, zitatimia.

Kwa hiyo, naomba sana ridhaa zenu mniruhusu kufanya hiyo kazi. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Riziki Pembe Juma. Waheshimiwa Wajumbe nadhani mmeshamsikia Mhe. Riziki Pembe Juma akijieleza. Kwa hiyo, mimi naomba nitoe nafasi kama kuna yeyote ana suali. Kama kuna maswali yasiozidi matatu ili aweze kuulizwa Mheshimiwa baada ya hapo tuweze kuendelea na shughuli zetu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nilikuwa nataka kumuuliza mgombea suala dogo sana. Kwa sababu kina mama wameamka sana katika kuendeleza uongozi na tukiwapa uongozi wanakuwa makini sana. Nilitaka kujua tu elimu yako au uzoefu wako uliopata ili basi tukupe ridhaa ya kuongoza katika Baraza hili. (*Makofi*)

Mhe. Riziki Pembe Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kulijibu suali la Mhe. Mohammed Said Mohammed kama ifuatavyo kama alivyosema kwa ufupi sana.

Elimu yangu kwa ufupi sana nina shahada ya pili yaani ni *Masters*, lakini ni Shahada ya pili kwa lugha yetu ya Kiswahili na nilipata Shahada yangu hii katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, labda nitamuongezea zaidi kwamba

mbali ya hiyo Shahada ya pili, lakini pia nilikuwa mwalimu katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar SUZA. *(Makofi)*

Mbali ya hayo nimeshiriki ama nimefanya kazi nyingi za wanawake ikiwemo mojawapo nimeshiriki Makongamano ya wanawake wanaita *WAFA Women Academy For Africa*, nimeshiriki mara mbili, tulifanya moja Nairobi lakini na la pili tulilifanya Uganda, lakini pia nimepata fursa ya kushiriki hayo hayo maendeleo ya wanawake kupitia umoja wa vijana UVCCM tulikwenda Hungary, nilikwenda kuwakilisha kundi la wanawake kutoka Vijana na kwa bahati nzuri sana kufika kule nilifunzwa mengi kuhusu wanawake, na ikaja kwamba ile *Women we can do it. (Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani mnaona kwamba tunaweza, kwa hivyo, kwa hilo wala usiwa na shaka Mhe. Mwakilishi, nitalifanya vizuri na kwa sababu uzoefu huo ninao na nadhani pengine itakuwa tunaelewana kwa sababu ndio wanawake tumo baadhi yetu tunakutana katika zile harakati zetu za wanawake. Kwa hivyo, kwa suala hilo halina mashaka, nitalifanya vizuri na nitalisimamia vizuri kwa sababu wanawake tunaweza. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe Riziki, suali jengine kama lipo.

Waheshimiwa Wajumbe: Maaruf, Maaruf *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Riziki Pembe Juma, tafadhali. Sasa nichukue nafasi hii kumuita mbele yenu Mhe. Shehe Hamad Mattar, tafadhali. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Mattar, mbele yako ni Wawakilishi, utajieleza kwa kiasi cha kama dakika tatu hivi kujieleza, baada ya hapo nitawaruhusu wakuulize maswali yasiyozidi matatu, tafadhali.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, Mheshimiwa Kiongozi wa Serikali katika Baraza, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar, mabini na mabwana *Asalamu Alaykum.*

Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kufika katika chombo hichi kikubwa cha Zanzibar au cha Taifa tukiwa wazima na salama, pia, sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mimi binafsi kuingia katika chombo hichi ambacho nilikuwa nakitafuta kwa hamu tokea mwaka 2000 nagombea nafasi hii, leo 2016 Mwenyezi Mungu amenipa nafasi hii. *(Makofi)*

Pia, niendelee kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni Pemba ambaokuwa wameniamini na kunipa kura zao na kufika katika chombo hichi. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, nimesimama hapa kwa ajili ya kuomba nafasi hii ya Mwenyekiti wa Baraza kwa lengo la kukitumikia chombo hichi cha Taifa, ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika maisha yangu katika Zanzibar hii ili kuona inasonga mbele. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nafasi hii nimeiomba kwa sababu naona Mwenyezi Mungu mara nyingi sana kila ninapofika katika taasisi au chombo bila ya kujitambua wananchi wananiamini kunipa nafasi ya Mwenyekiti, lakini leo katika chombo hichi kikubwa pia wenzangu wananiamini, kwa hivyo, ni imani yangu kwa mashirikiano basi nitaweza kuendesha chombo hichi kwa salama na amani kifikie tunakokusudia.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, sitaki niwachoshe sana kubwa nawaomba kura zenu za ndio zote na pia nawaomba mashirikiano yetu. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar, Waheshimiwa Wajumbe, tumemsikia Mhe. Shehe Hamad Mattar, akijieleza sasa naomba nikupeni nafasi sasa na nyinyi kama kuna yoyote mwenye suali ili aweze kumuuliza. Maswali?

Waheshimiwa Wajumbe: Maaruf, Maaruf *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Shehe Hamad Mattar, tafadhali, sana. Waheshimiwa Wajumbe, tumeshawasikia wenzetu wakijieleza kwa nafasi zote tatu, ikitanguliwa na nafasi ya Mheshimiwa Naibu Spika, na hizi mbili za wenyeviti. Sasa naomba nichukue nafasi hii nimuite Katibu ili waanze kufanya utaratibu wa kura. Katibu tafadhali.
Katibu: Mhe. Spika, nawaomba wenzangu wanipe idadi ya Waheshimiwa Wajumbe waliomo ndani ya ukumbi na wakati huo huo tuanze kugawa *ballot papers*, waheshimiwa narudia kusema kwamba *ballot paper* ya mgombea wa

Naibu Spika, ni moja na ina alama ya ndio au hapana, mjumbe anaomba ridhaa yenu na kwa hivyo, utaweka ama 'ndio' ama 'hapana', kwenye *ballot paper* ya Wenyeviti kuna wagombea wawili, wanaohitajika ni wote wawili, kwa hivyo, onyesha ridhaa yako kwa wote, wagombea wawili tuna nafasi mbili, kwa hivyo, kila mmoja anaweka alama ya 'ndiyo' au 'hapana' kwa kila mmoja. Baadae tutaanza kuzikusanya kura za Mhe. Naibu Spika, na nyengine baadae za Wenyeviti naomba nipewe idadi ili nitangaze kuna wajumbe wangapi ndani.

Mhe. Spika, wenzangu wananiambia kuna Wajumbe sabini na nne (74) ndani ya Ukumbi na kwa ruhusa yako tunakuomba kwa heshima na taadhima uturuhusu tuanze kugawa *ballot papers* kwa ajili ya uchaguzi, naomba watendaji wenzangu mugawe hilo karatasi za kura.

Mhe. Spika: Naomba muanze kugawa karatasi za kura.

(Hapa karatasi za kura za Mgombea Naibu Spika zilianza kugawiwa kwa Wajumbe)

Katibu: Waheshimiwa, mukiwa tayari tutaanza kukusanya zile *ballot papers* za mgombea wa nafasi ya Naibu Spika, nafikiri tutatumia moja tu, basi kwanza hiyo moja tuache kwa sababu ya kusubiria Wenyeviti, kwa hivyo, naomba upite kukusanya hizo kura, tunakusanya moja tu ya Naibu Spika.

Waheshimiwa, tunaweka *box* jengine na toa hilo weka pale, hatutotoa kura Waheshimiwa tutatoa ile karatasi ya nje. Mhe. Spika, nimeona nitoe maelekezo zaidi ya kura hizi za Mwenyekiti, tunasema kwamba nafasi ni mbili; tumepata majina ya wagombea wawili, kwa hiyo, mnachotakiwa Waheshimiwa Wajumbe ni kuonyesha ridhaa zenu kwa kila mgombea, onyesha alama ya 'ndio' au 'hapana' kwa kila mgombea. Kwa hivyo, tunategemea kwenye *ballot* yako hiyo utakuwa umeweka alama mbili; alama moja kwa kila mgombea.

(Hapa karatasi za kura za wagombea Wenyeviti zilianza kugawiwa kwa Wajumbe)

Katibu: Mhe. Spika, naomba nikupe taarifa kwamba zoezi la kukusanya kura limekamilika kwa heshima na taadhima nikuombe sasa uliahirishe Baraza lako kwa muda wa nusu saa ili tuende kuhesabu kura na kurudi baada ya hiyo nusu saa ili kutangaza matokeo Mhe. Spika, tafadhali.

Mhe. Spika: Ahsante Katibu, labda kwanza kabla sijafanya shughuli ya kusitisha, ningewaomba wagombea kila mmoja aweze kuleta jina la wakala wa kuweza kwenda kusimamia kura zake na kwa mantiki hiyo nitaanza na mgombea wa nafasi ya Naibu Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante Mhe. Spika, mimi wakala wangu atakuwa Mhe. Wanu Hafidh Ameir.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Nafasi ya Mwenyekiti nikianza na Mhe. Riziki Juma Kona.

Mhe. Riziki Pembe Juma: Ahsante Mhe. Spika, mimi namchagua Mhe. Mwanaasha Khamis Juma. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sasa nampa nafasi Mhe. Shehe Hamad Matar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, mimi namchagua Mhe. Rashid Ali Juma wa Jimbo la Amani. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa baada ya shughuli hiyo nitawaomba Katibu aweze kuwaruhusu watu wake waondoke na hizo *ballot papers* pamoja na mawakala wa Waheshimiwa.

Baada ya shughuli hiyo, naomba sasa nisitishe shughuli za Baraza la Wawakilishi kwa muda usiozidi nusu saa ili kuwapa nafasi waweze kuhesabu hizo kura na baada ya hapo tutarudi ili kuja kutoa taarifa za matokeo na mambo mengine yatakayofuata.

(Saa 3.39 Asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka baada ya kuhesabu kura)

(Saa 4:20 Baraza lilirudia)

MATOKEO YA UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA NA WENYEVITI

Katibu: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima sasa tuko tayari kutoa matokeo ya uchaguzi uliofanyika muda mchache uliopita. Tukianza na uchaguzi wa nafasi ya Mhe. Naibu Spika, kama tulivyosema mgombea alikuwa ni mmoja Mhe. Mgeni Hassan Juma, wajumbe waliopiga kura ni 74, kura 1 imeharibika na imeharibika katika namna ile ile ya juzi, kuna Mjumbe amerudisha *ballot* haikupigwa kura. Kwa hiyo, kura ambazo zilikuwa ni sahihi ni 73, kura 1 imemkataa na kura 72 zimemkubali mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa mamlaka niliyopewa sasa naomba niwatangazie mshindi wa nafasi ya Unaibu Spika, mshindi huyu atapatikana kwa mujibu wa Kanuni ya 8(2) (c) ambayo inafanya marejeo ya Kanuni ya 5(i) inayoeleza kuwa mshindi wa nafasi ya Uspika atapatikana kwa kura zaidi ya nusu ya wajumbe waliopigiwa kura. Kwa hiyo, napenda sana sasa kumtangaza mheshimiwa kuwa Naibu wetu Spika mpya, mheshimiwa karibu sana. (*Makofi*)

Mhe. Mgeni Hassan Juma anakuwa mshindi wetu wa nafasi ya Naibu Spika. (*Makofi*)

Katibu: Mhe. Spika, kwenye kura za Wenyeviti tulikuwa na wagombea wawili, mgombea wa kwanza ni Mhe. Riziki Pembe Juma. Wajumbe waliopiga kura ni Wajumbe 74, kura 1 tena imeharibika, kura 73 ndio zimekuwa ni kura halali na kura zote 73 zimemkubali Mhe. Riziki Pembe Juma. (*Makofi*)

Mgombea mwengine wa kiti hicho alikuwa ni Mhe. Shehe Hamad Mattar. Wajumbe ambao wamempigia kura ni 74, kura 1 imeharibika, kura halali zimebaki ni 73 na kura zote 73 zimemkubali Mhe. Shehe Hamad Mattar. Mheshimiwa naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa matokeo hayo na kwa mujibu wa mamlaka niliyopewa Mwenyekiti wa Baraza atapatikana kwa kupata kura zaidi ya nusu za Wajumbe walioshiriki katika uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni ya 5(i), 8(2)(c) na Kanuni ya 10 (1). Kwa mantiki hiyo sasa napenda niwatangaze Mhe. Riziki Pembe Juma na Mhe. Shehe Hamad Mattar kuwa Wenyeviti wetu wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Sasa labda kabla hatujaendelea kwenye shughuli nyengine naomba niwape nafasi chache sana wagombea ili waweze kutoa neno la shukurani, nikianza na mgombea kwa nafasi ya Naibu Spika, ambaye sasa hivi amekuwa ni Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma tafadhali kama kuna lolote la kuzungumza.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, ahsante sana nichukue fursa hii adhimu kwanza kukushukuru wewe Mhe. Spika kwa kuweza kuendesha shughuli yetu hii ya leo ya uchaguzi. Lakini pia nichukue fursa hii adhimu kuwashukuru wajumbe wote ambao wamenipigia kura aidha ya kunikubali hata wale ambao wameharibu na hata yule ambaye amenikataa. (*Makofi*)

Mimi naahidi kwamba nitafanya kazi kwa mashirikiano na Wajumbe wote ndani ya Baraza hili bila ya kumbagua mtu yeyote, lakini pale ambapo nitakaposhauriwa basi nitakuwa tayari kushaurika.

Vile vile nitafanya kazi na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi ambao mara nyingi huwa tunawahitaji sana katika shughuli zetu, basi nisichukue muda mrefu sana kuzungumza. Mimi nashukuru sana kwa kura zenu na mumenijengea uwezo wa kujiamini hasa kwa kuwa mumenichagua kwa kura nyingi sana. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa hilo neno lako la shukurani, sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti wa mwanzo hapa kwenye orodha yangu Mhe. Riziki Pembe Juma ili na yeye aweze kutoa neno lake la shukurani, tafadhali.

Mhe. Riziki Pembe Juma: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kweli sitokuwa na maneno mengi ya kusema zaidi nitasema ahsanteni sana. Ninawaahidi kwamba tutafanya kazi kwa pamoja kwa kushirikiana kwa maendeleo ya Baraza, nchi na Taifa letu kwa ujumla. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Riziki Pembe Juma. Sasa nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar na yeye tuweze kusikia neno lake, tafadhali.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, ahsante kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kushukuriwa kwa kutujaalia utulivu katika uhai, uzima na utulivu katika Baraza tukaweza kuendesha uchaguzi wetu kwa salama na amani na matokeo yakawa mazuri. Nikushukuru wewe Mhe. Spika pamoja na Wajumbe wa Baraza hili kwa imani yao waliyoanza kunionesha tokea hapo mwanzo, nawaahidi kwamba sitawaangusha kama walivyokuwa hawakuniangusha.

Pia nawaahidi tena kwamba mimi natokea kwenye Jumuiya ya Wazazi kwa hivyo ni mlezi, nitalea Baraza zima *inshaallah*. Na nitakuwa tayari kujikosoa na kukosolewa na kupokea ushauri wenu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa neno la shukurani.

Waheshimiwa Wajumbe, mimi nitoe pongezi zangu za jumla za dhati kwenu nyote kwa kushiriki kwenye suala hili la uchaguzi wa Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wetu na kila mmoja amefanya lile ambalo ni haki yake Kikatiba. Wako ambao wameharibu kura ni mambo ya kawaida, kuna kura moja ambayo imekataa naye pia katimiza wajibu wake. Kwa hiyo, mimi niwapongeze wote kwa pamoja kwa kuweza kufanikisha hili zoezi.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaanza na utaratibu wa kuahirisha hizi shughuli zetu kwa leo nimepata barua hapa inatoka kwa Mhe. Spika Mstaafu ambayo ameniandikia mimi, lakini pia amekuandikieni nyinyi. Kwa hivyo, hii barua ni kwa ajili yetu sote mimi pamoja na nyinyi, hivyo kwa heshima zote naomba niisome mbele yenu ili tuweze kupokea huu ujumbe wa taarifa ya Mhe. Spika Mstaafu. Ni ya leo tarehe 01 Aprili, 2016 anani-*address:*

"Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi na kila vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia nchi yetu kuwa bado ni salama ikiwa ni pamoja na mshikamano uliokuwepo. Jambo ambalo limeiwezesha kumaliza kwa uchaguzi wetu kwa amani na kuwapata viongozi tuliowachagua wenyewe kwa njia ya kidemokrasia.

Pili, naomba niwashukuru sana viongozi wa chama changu cha CCM kuanzia Kamati Kuu, Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM, Zanzibar kwa kuendesha mchakato wa kumpata Spika vizuri.

Ninawashukuru mno Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wale waliokuwa wa Baraza la Tano, Baraza la Sita, Baraza la Saba na Baraza la Nane kwa imani yao kubwa waliyonionesha, si tu ya kunichagua kuyaongoza Mabaraza hayo, bali pia kwa kunipa mashirikiano makubwa yaliyoniwezesha kufanya kazi yangu hiyo kwa wepesi.

Mhe. Spika, naomba pia nikupongeze wewe binafsi kwa dhati kabisa kwa kuchaguliwa katika nafasi hiyo kwa ushindi wa kishindo. Imani ya chama chetu na imani ya Wajumbe wa Baraza la Tisa la Wawakilishi ni kubwa sana juu yako kwamba utakiongoza chombo hiki kitukufu kwa busara, hekima na uweledi mkubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie nguvu na busara katika uongozi wako. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii adhimu kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar kwa kupata fursa hii ya kuwawakilisha wananchi. Kazi hii waliyoiomba na kuipata kwa ridhaa ya wananchi ni jukumu kubwa ambalo linabaki kuwa ni deni kwa waliowachagua. Ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasaidie na awaongoze katika kila jambo la kheri katika kutekeleza majukumu yenu Kikatiba. Zaidi naomba Waheshimiwa Wajumbe wakupe ushirikiano wa dhati ili uweze kutekeleza shughuli zako kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, naomba unifikishie shukurani zangu za dhati kwa Katibu na watumishi wote wa Baraza kwa ushirikiano mkubwa walionipa muda wote ambao tumekuwa tukifanya kazi zetu kwa pamoja. Wamenisaidia sana katika kukiongoza chombo hiki kitukufu, uzoefu na elimu zao kwangu vilikuwa ni darasa tosha katika kukabiliana na changamoto mbali mbali. Nawaomba watumishi wote wakupe ushirikiano wa kutosha.

Mhe. Spika, mwisho naomba niishukuru familia yangu kwa utulivu na ustahamilivu mkubwa waliyonionesha katika kipindi chote ambacho nimekuwa kiongozi wa chombo hiki. Uvumilivu wao ulikuwa ni faraja ambayo imenipa nguvu ya kuweza kuitumikia nafasi hiyo. Nawashukuru sana na ninaliombea kila la kheri na baraka nyingi Baraza hili tukufu la Tisa na Mwenyezi Mungu awasaidie. Amiin."

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo kwanza nadhani nimpe Mhe. Mwanasheria Mkuu kama kuna hoja yoyote inataka kutolewa.

Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa kuwa orodha ya shughuli za leo zilizopangwa zimemalizika na hakuna shughuli nyengine ya jioni, naomba kutoa hoja ya kutenga kando Kanuni ya 23 ili tuahirishe kikao hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 04/04/2016 saa 3:00 za asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante hoja imetolewa na naona imeungwa mkono. Sasa naomba nichukue nafasi hii kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wote ambao wanaiunga mkono hoja hii wanyanyue mikono, wale wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha naomba nitoe matangazo ambayo yamefika mezani kwangu.

Kwanza kabisa kuna tangazo niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wanawake wote kubakia ukumbini mara baada ya kuahirishwa kwa kikao cha leo, kuna mambo muhimu wanayotakiwa kuyajadili.

Kuna tangazo vile vile inaonekana linatoka sehemu ya Utumishi, Waheshimiwa wote waliowasilisha nambari za *account* ambazo si za Benki ya *PBZ* munaombwa mfike *Division* ya Utumishi baadae.

Waheshimiwa Wajumbe, mnatakiwa mara baada ya kuahirishwa kikao hiki, mfike katika ukumbi wa juu wa mikutano kwa ajili ya kupata maelezo na taarifa mbali mbali zinazohusu huduma za kibenki kutoka kwa benki zifuatazo. *NMB, Postal Bank* na *CRDB*. Waheshimiwa munaombwa kuhudhuria bila ya kukosa.

Tanganzo la mwisho ni tangazo kwamba Wajumbe wote watakaopendelea kufanya mazoezi, mnaombwa mujiandikishe majina yenu kwa Mhe. Wanu Hafidh Ameir. (*Makofi*)

Baada ya matangazo hayo sasa naomba niahirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatatu, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 5:00 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 04/04/2016 saa 3:00 asubuhi)